JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI 2022/23 - 2025/26

Novemba, 2022

# MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI 2022/23 - 2025/26

**Imeandaliwa Na:**

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Rais TAMISEMI**

**Novemba, 2022**

# YALIYOMO

**YALIYOMO**………………………………………………………….. i
**DIBAJI**……………………………………………………................ iii
**VIFUPISHO**……………………………………………………..……. iv
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**………………………….…….. 1
**1.Usuli**……………………………………………………….………. 1
**1.1. Umuhimu wa Ngazi ya Msingi Katika Kuwaletea Wananchi Maendeleo**……………………………….……. 1
**1.2. Hali Halisi**…………………………………………..……... 2
**1.2.1. Juhudi za Kitaifa katika Kuboresha Utendaji Kazi na Utoaji wa Huduma Ngazi ya Msingi**…………………...... 2
**1.2.2.Changamoto**..........................................................…. 6

**SURA YA PILI:MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI**……..... 9
2.0 Utangulizi……………………………………………… 9
2.1 Umuhimu wa Mpango……………………………… 9
2.2 Dira……………………………………………..……… 10
2.3 Dhima………………………………………………………10
2.4 Lengo……………………………………………………....10
2.4.1 Lengo Kuu……………………………………………...10
2.4.2 Malengo Mahsusi……………………………………...10
2.5 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango………………………10
2.6 Shabaha za Mpango……………………………………... 11
2.7 Viashiria vya Matokeo ya Mpango………………………… 11
2.7.1 Viashiria vya muda mfupi……………………………..11
2.7.2 Viashiria vya Matokeo ya Muda Mrefu………………………12
2.8 Mbinu/Njia za Utekelezaji…………………………..….....12

**SURA YA TATU: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI**…………………………………….……………. 14
3.0 Utangulizi……………………………………….…….. 14
3.1 Utekelezaji wa Mpango………………………………… 15
3.2 Matokeo ya Utekelezaji wa Mpango…………………… 17

**SURA YA NNE: GHARAMA ZA UTEKELEZAJ……………….. 18**
4.0 Utangulizi………………………………………………… 18
4.1 Gharama za Utekelezaji wa Mpango……………………. 18

**SURA YA TANO: MUUNDO WA KITAASISI NA URATIBU WA MPANGO…………………………………………….…... 20**
5.0 MUUNDO WA KAMATI……………………………………. **20**
5.1 Kamati Makatibu Wakuu…………………………….…..… **20**
5.2 Kamati ya Wataalam……………………………………….. **21**
5.3 Kamati ya Uratibu Ngazi ya Mkoa………………………… **21**
5.4 Kamati ya Uratibu Ngazi ya Halmashauri………….......... **22**
5.5 Ngazi ya Tarafa……………………………………………… **23**
5.6 Timu ya Wataalam Ngazi ya Kata…………….……….. **24**

**SURA YA SITA: UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MPANGO………………………………………………….…... 25**
6.0 Utangulizi…………………………………………………….. 25
6.1 Malengo ya Ufuatialiji wa Mpango……………………….. 25
6.2 Viashiria na Shabaha……………………………….……. 26
6.3 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtiririko na Taarifa……….……. 26

**ORODHA YA MAJEDWALI**

JEDWALI NA.1: MPANGO KAZI……………………………. ………. 20
JEDWALI NA.2: BAJETI YA MPANGO………………………………….. 24
JEDWALI NA. 3: MPANGO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI……………… 43

# DIBAJI

Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo ngazi ya msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 umeandaliwa kwa ajili ya kuwezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo ngazi ya jamii na Taifa kwa kutumia rasilimali walizonazo katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kufuatilia shughuli za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira.

Mpango unalenga kuchochea na kufanya mageuzi ya kifikra, mtazamo na kiutendaji kwa timu ya wataalam ngazi ya Kata, Halmashauri, Mkoa na Wizara ili kuboresha utendaji na utoaji wa huduma katika sekta mbalimbali. Aidha, yatafanyika maboresho ambayo yatawezesha kuwa na timu ya wataalamu wenye weledi, stadi, vifaa, vitendea kazi, rasilimali fedha na mifumo ya uratibu na ufuatiliaji katika Ngazi ya Kata.

Utekelezaji wa Mpango huu:- utaimarisha uwezo wa watendaji wa Serikali katika ngazi ya Msingi; utaimarisha uwezo wa jamii kutatua changamoto zinazoikabili kwa kutumia rasilimali zilizopo bila kuisubiri serikali; utaongeza uwezo wa jamii kusimamia na kuelezea manufaa ya miradi ngazi ya jamii na kitaifa; utapanua wigo wa wananchi kuwasiliana na Serikali ngazi ya kijiji/Mtaa hadi taifa; utaongeza uwezo wa wataalam kutumia TEHAMA na njia za kisasa za mawasiliano kuibua fursa na kutatua changamoto katika maeneo na hatimaye kuboresha huduma zinazotolewa kwa jamii.

**Prof. Riziki Shemdoe**
**Katibu Mkuu OR TAMISEMI**

**Dkt Zainab S. Chaula**
**Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **BRELA** | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **OR-MUUUB** | Ofisi ya Rais, Manejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| **OWM** | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| **O & OD** | Opportunity and Obstacle to Development ***"Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo"*** |
| **RLGSP** | Programu ya kuimarisha Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **REA** | Wakala wa Nishati Vijijini |
| **RUWASA** | Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijni |
| **TARURA** | Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini |
| **TANROADS** | Wakala wa Barabara Tanzania |
| **TANESCO** | Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania |
| **TASAF** | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania |
| **TBC** | Shirika la Utangazaji Tanzania |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **WDC** | Kikao cha Maendeleo ya Kata |
| **WEST** | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| **WHMTH** | Wizara ya Habari, Mawasilano na Teknolojia ya Habari |
| **WMJJWM** | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum |
| **ZUSE** | Zungumza na Serikali |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1. Usuli

Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo ngazi ya msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 umeandaliwa kwa ajili ya kuwezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo ngazi ya jamii na Taifa kwa kutumia rasilimali walizonazo katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kufuatilia shughuli za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira. Wananchi wanatakiwa kutambua nafasi zao katika jamii, kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo, kudai haki za msingi, kuhakikisha viongozi wanatimiza wajibu wao ipasavyo na kuwajibika.

Mpango unalenga kuchochea na kufanya mageuzi ya kifikra, mtazamo na kiutendaji kwa timu ya wataalam ngazi ya Kata ili kuboresha utendaji na utoaji wa huduma katika sekta za elimu, afya, maji, nishati, mawasiliano, usafiri na usafirishaji, misitu na mazingira, ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii, uongozi na utawala bora. Aidha, maboresho katika utendaji na utoaji wa huduma yatawezesha kuwa na timu ya wataalamu wenye weledi, stadi, vifaa, vitendea kazi, rasilimali fedha na mifumo ya uratibu na ufuatiliaji. Matokeo ya utekelezaji wa mpango yanategemewa kutolewa taarifa na mrejesho kupitia mijadala, mikutano, vyombo vya Habari, mifumo ya TEHAMA na njia za kisasa za mawasiliano kama vile *blogs, Twitter, Facebook, Youtube na Hash Tag.*

### 1.1. Umuhimu wa Ngazi ya Msingi Katika Kuwaletea Wananchi Maendeleo

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, Ibara ya 145 na 146, Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi ambavyo vipo

katika ngazi za chini za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyombo hivi huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe. Serikali za Mitaa huwezesha wananchi kuwa na sauti katika maamuzi mbalimbali na kushiriki moja kwa moja katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

Moja ya jukumu la msingi la Serikali kwa wananchi ni kuboresha na kutoa huduma kwa wananchi. Huduma hizi hutolewa kupitia sekta za elimu, afya, maji, nishati, Mawasiliano, usafiri na usafirishaji, misitu na mazingira, ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii, uongozi na utawala bora. Ili huduma hizi zitolewe kwa ufanisi ngazi za msingi zinapaswa kuwa na wataalamu wenye weledi, stadi, vifaa, vitendea kazi, rasilimali fedha na mifumo ya uratibu na ufuatiliaji.

## 1.2. Hali Halisi

Serikali imeendelea kufanya maboresho mbalimbali katika maeneo ya Sera, Sheria, Miongozo, Miundo na mifumo ili kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi katika ngazi ya msingi. Maboresho hayo yamepanua wigo wa wananchi kushiriki katika kujiletea maendeleo yao kwa kutumia rasilimali walizonazo na msaada wa kiutaalam. Juhudi mbali mbali zinazoendelea kufanyika na changamoto zinazohitajika kutatuliwa ili kufikia lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji huduma ngazi ya msingi ni kama ifuatavyo:-.

### 1.2.1. Juhudi za Kitaifa katika Kuboresha Utendaji Kazi na Utoaji wa Huduma Katika Ngazi ya Msingi

Serikali inaendelea kufanya maboresho mbalimbali katika maeneo ya Sera, Sheria, Miongozo, Miundo na Mifumo ili

kuhakikisha jamii inashiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira kama ifuatavyo:-

**(i) Sera na Sheria**

Serikali katika kutengeneza mazingira wezeshi ya ushiriki wa wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo imeandaa Sera, Sheria na miongozo mbalimbali kama vile:- Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996, Andiko la Sera ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1998 kuhusu ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi, Sera ya Misitu ya Mwaka 1998, Sera ya Maji ya Mwaka 2002, Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sera ya Kilimo ya Mwaka 2019, Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021, Sheria ya Huduma za Habari, Na.12 ya mwaka 2016 na Sheria ya Haki ya Kupata taarifa mwaka ya 2016.

**(ii) Miundo**

Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ni moja ya nyenzo ya kuwafikia wananchi katika utekelezaji wa kazi za kila siku. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina ngazi kuu mbili za utawala ambazo ni Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Serikali Kuu hujumuisha Wizara, Idara, Taasisi zinazojitegemea, Mikoa, Wilaya na Tarafa. Serikali za Mitaa hujumuisha Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji. Mpango huu unalenga kuimarisha ngazi ya Kata ambayo ndiyo ngazi muhimu ya kuwaunganisha wanachi katika vijiji/mitaa na serikali.

Tarafa ni ngazi ya chini ya kiutawala ya Serikali Kuu ambayo ipo kati ya Wilaya na Kata. Ofisi ya Tarafa huongozwa na Afisa Tarafa ambaye majukumu yake ni pamoja na:- kumwakilisha na

kumsaidia Mkuu wa Wilaya katika utekelezaji wa shughuli za Serikali Kuu katika Tarafa, kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye shughuli za maendeleo na kuwa kiungo kati ya Serikali kuu na Wananchi katika Tarafa. Majukumu haya yanaendana na utekelezaji wa mpango huu.

Kata ni ngazi ya msingi ya utawala wa nchi na ziko chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zinaweza kuwa Jiji, Manispaa, Halmashauri za Wilaya au Miji. Kata huongozwa na Afisa Mtendaji wa Kata ambaye husaidiwa na timu ya wataalam **(Ward Management Team-(WMT))** akiwemo Afisa Maendeleo ya Jamii, Mratibu Elimu wa Kata, Wagani wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Afisa Ustawi wa jamii, na Afisa Afya. Ofisi ya Kata ni kiungo muhimu chenye wataalam ambao wana uwezo wa kutoa utalaam na kutatua changamoto za wananchi kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji/Mitaa.

**Majukumu ya Timu ya Wataalam katika Ngazi ya Kata**

Kwa mujibu wa muundo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa wa mwaka 2022, ngazi ya Kata inajumuisha wataalamu wa sekta mbalimbali. Wataalam hao wanatumika kama timu ya uwezeshaji wa shughuli za kijamii, kiuchumi, Kiutamaduni na Kimazingira na huwajibika kutoa taarifa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata ambayo imeanzishwa kwa mujibu Kifungu Namba 31 cha Sheria Namba 7 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 6 ya mwaka 1999.

### (iii) Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD)

Mfumo wa O&OD ulizinduliwa mwaka 2001 kama njia ya kuwashirikisha wananchi katika uandaaji wa mipango ya maendeleo inayoanzia katika ngazi ya jamii. Mwaka 2010 mfumo ulirasimishwa kuwa mfumo shirikishi wa upangaji mipango na bajeti katika Mamlaka za serikali za Mitaa kuanzia

ngazi za msingi. Aidha, mwaka 2019 mfumo ulifanyiwa maboresho kwa lengo la kuhamasisha jitihada za jamii, kuziendeleza na kuimarisha ushirikiano ili kufikia utoaji huduma bora kwa kuamsha ari ya wananchi kushiriki kwenye shughuli za maendeleo katika ngazi za msingi.

Mfumo huu ni toshelezi kwa kuwa unajenga mahusiano baina ya Serikali na jamii kwa kuimarisha uwezo wa wataalam katika ngazi ya Kata katika kubaini na kutia moyo uanzishwaji wa jitihada za jamii, kuzijengea uwezo jamii kutekeleza na kukamilisha jitihada hizo. Katika mfumo huu, ajenda ya uwezeshaji ni endelevu kwa kuwa inaibua na kuendeleza wawezeshaji ngazi ya jamii wakati wote wa mchakato wa maendeleo ya jamii. Uwezeshaji huo unaanza katika ngazi ya Kata kupitia wawezeshaji ambao ndiyo wanaunda Timu ya watalaamu ngazi hiyo.

**Majukumu ya Timu ya Wataalam wa Kata Katika Mfumo wa O&OD**

i. Kusaidia jamii kutambua fursa walizonazo, changamoto na kupanga namna ya kuzikabili;
ii. Kushirikiana kwa pamoja na viongozi wa Kijiji/Mtaa na jamii katika kufuatilia na kutathmini shughuli za maendeleo kutoka ngazi ya Kijiji hadi Kitongoji;
iii. Kusaidia jamii kujijengea uwezo wa kujifunza kupitia uzoefu katika utekelezaji wa jitihada mbalimbali;
iv. Kutoa usaidizi wa kitaalam kupitia taaluma zao na kuwasiliana na Mtendaji Kata na Kikosi Kazi cha Halmashauri katika kutatua changamoto zilizo nje ya uwezo wa Wawezeshaji Kata;
v. Kuwatambua, kuwajengea uwezo na kuwalea Wawezeshaji Jamii kwa ajili ya maendeleo endelevu;
vi. Kuwa kiungo kati ya jamii na wadau wengine katika kuunga mkono juhudi za jamii kujiletea maendeleo; na
vii. Kutoa uzoefu wa uwezeshaji katika vikao mbalimbali kama vile Kikao cha Maendeleo ya Kata ili kuongeza uelewa wa Uwezeshaji Jamii na kukuza juhudi za jamii husika kujiletea maendeleo.

Pamoja na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali bado zipo changamoto mbalimbali zinazoathiri matokeo tarajiwa. Tathmini inaonyesha kuwa changamoto hizi zinatokana na sababu mbalimbali zifuatazo:-

### 1.2.2. Changamoto

**a) Upungufu wa wataalam ngazi ya Kata**

Mahitaji ya wataalam wanaohitajika katika ngazi ya kata ni **23,706** ambapo waliopo ni **17,265** na upungufu ni wataalam **6,368** sawa na asilimia **26.8** kama ilivyoanishwa katika jedwali namba 1.

**Jedwali Na.1 Idadi ya Wataalam Ngazi ya Kata**

| Na | Kada | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | % ya Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| **i.** | Watendaji wa Kata | 3,956 | 3,694 | 262 | 6.6 |
| **ii.** | Maafisa Maendeleo ya Jamii[1] | 3,956 | 1658 | 2,225 | 56.2 |
| **iii.** | Maafisa Kilimo | 3,956 | 3956 | 0 | 0 |
| **iv.** | Maafisa Mifugo | 3,956 | 3642 | 314 | 7.9 |
| **v.** | Maafisa Elimu Kata | 3926 | 3926 | 0 | 0 |
| **vi.** | Maafisa Uvuvi | 3,956 | 389 | 3,567 | 90.1 |
| **vii.** | Waganga Wafawidhi wa Vituo[2] | | | | |
| | **Jumla** | **23,706** | **17,265** | **6,368** | **26.8** |

[1] Kwa upande wa Mkoa mahitaji ni 52, waliopo 47 na upungufu ni 5. Ngazi ya Halmashauri makao makuu mahitaji 1288, waliopo ni 1358, ziada ni 70. Ngazi ya Kata mahitaji ni 3,956, waliopo ni 1,664 na upungufu 2,295, hivyo baada ya kufanya masawazo ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata kutakuwa na upungufu 2,225.

[2] Waganga wafawidhi wa Vituo si lazima wawepo kila Kata isipokuwa wanapangwa kimkakati kwenye maeneo ya Kata

## b) Upungufu wa Ofisi za Tarafa na Kata

Mahitaji yaOfisi za Tarafa **21,107** ambapo zilizopo ni **7,539** na upungufu ni ofisi **13,568** sawa na asilimia **64** kama ilivyoanishwa katika jedwali namba 2.

**Jedwali Na.2: Ofisi za Tarafa na Kata**

| Na. | Aina ya Ofisi | Mahitaji | Ilizopo | Upungufu | %ya upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| **I** | Tarafa | 570 | 233 | 337 | 59.1 |
| **Ii** | Kata | 3,956 | 1,991 | 1,965 | 49.6 |
| **Iii** | Vijiji | 12,318 | 4,473 | 7,845 | 63.6 |
| **Iv** | Mitaa | 4,263 | 842 | 3,421 | 80.2 |
| | **Jumla** | **21,107** | **7,539** | **13,568** | **64** |

## c) Upungufu wa vyombo vya usafiri Wataalam ngazi ya Kata

Mahitaji ya pikipiki za uratibu katika ofisi za kata ni **15,824** ambapo zilizopo ni **3,790** na upungufu ni ofisi **12,304** sawa na asilimia **76** kama ilivyoanishwa katika jedwali namba 3.

**Jedwali Na.3: Vyombo vya Usafiri (Pikipiki)**

| Na. | Kada | Mahitaji | zilizopo | Upungufu | % ya upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| **i.** | Watendaji wa Kata | 3,956 | 711 | 3,245 | 82 |
| **ii.** | Maafisa Maendeleo ya Jamii | 3,956 | 29 | 3,927 | 99.2 |
| **iii.** | Maafisa Kilimo | 3,956 | 2,750 | 1,206 | 30.5 |
| **iv.** | Maafisa Mifugo | 3,956 | 300 | 3,656 | 92.4 |
| **v.** | Maafisa Uvuvi | | | | |
| | **Jumla** | **15,824** | **3,790** | **12,034** | **76** |

d) Upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo kwa wananchi katika ngazi vijiji/Mitaa na vitongoji

   Kutokuwepo na fedha za uhakika za kila mwezi za uendeshaji wa ofisi za kata, pamoja na kuwezesha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi katika ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji kama ilivyo kwa Maafisa Tarafa na Waratibu Elimu Kata.

e) Kukosekana kwa mrejesho juu ya masuala mbalimbali yanayoibuliwa na wananchi;

f) Mawasiliano duni baina ya viongozi wao kwa wao na kati yao na wananchi;

g) Viongozi wa ngazi za msingi kutotumika vema kuwezesha mawasiliano shirikishi na utekelezaji wa majukumu ya Serikali;

h) Uwezo hafifu wa viongozi na wataalamu wa ngazi za msingi kuwahudumia wananchi; na

i) Upungufu wa Maafisa Habari Ngazi ya Halmashauri.[3]

Kulingana na changamoto zilibainishwa ambazo zinafifisha utendaji na utoaji wa huduma ngazi upo umuhimu wa uwepo mpango wa kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma katika ngazi ya Kata.

[3] Mahitaji ya maafisa habari ni angalau moja kwa kila Halmashauri sawa na 184, waliopo ni 79 na upungufu 105 sawa na asilimia 57.

# SURA YA PILI

# MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza umuhimu wa mpango, dira, dhima, malengo, mikakati ya utekelezaji, shabaha za mpango, viashiria vya matokeo ya mpango, mbinu za utekelezaji wa mpango.

### 2.1 Umuhimu wa Mpango

Mpango unalenga kuchochea na kufanya mageuzi ya kifikra, mtazamo na utendaji wa wataalam ngazi ya Kata ili kuwezesha jamii kuwa kitovu cha maendeleo ngazi za Vijiji/Mitaa hadi Taifa. Serikali ya Awamu ya Sita (6) inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kuwezesha **wananchi kuwa kitovu cha maendeleo na kuimarisha ubia baina ya wananchi na** Serikali katika ngazi ya msingi. Hivyo, Mpango utawezesha:-

I. Kuimarisha ngazi ya Kata katika upatikanaji wa rasilimali watu yenye weledi, rasilimali fedha, vifaa, vitendea kazi na ofisi;
II. Kuamsha ari ya jamii kuhusu uzalendo, kufanya kazi kwa bidii na kujenga moyo wa kujitolea;
III. Jamii kuwa na mtazamo chanya katika kutekeleza mambo yao katika kupanga, kutekeleza, kusimamia na kujitathimini;
IV. Kuimarisha mahusiano ya kimashirikiano (Ubia) baina ya Jamii na Serikali;
V. Wananchi kuwasiliana na Serikali kuhusu masuala yanayogusa maisha yao na ustawi wao katika ya ngazi za msingi;

VI. Kuongeza kasi ya upatikanaji wa taarifa na kupata mrejesho kwa wakati; na

VII. Serikali kubaini changamoto zinazowakabili wananchi na kuweka mikakati ya pamoja kwa kushirikisha wananchi katika kutafuta majawabu ya changamoto.

### 2.2 Dira

Kuwa na mfumo shirikishi kwa ustawi na maendeleo ya jamii.

### 2.3 Dhima

Kuwezesha upatikanaji wa maendeleo na ustawi wa jamii kwa kuimarisha utendaji kazi ngazi za msingi za jamii.

### 2.4 Lengo

#### 2.4.1 Lengo Kuu

Kuimarisha mfumo wa utendaji kazi katika ngazi ya msingi na mawasiliano ngazi Vijiji/Mitaa hadi Taifa.

#### 2.4.2 Malengo Mahsusi

a) Kuimarisha uwezo wa wataalam wa Serikali kuanzia ngazi ya Mitaa/Vijiji, Kata, Tarafa, Halmashauri, Mkoa hadi Taifa katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

b) Kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

c) Kuongeza wigo wa wananchi kuwasiliana na Serikali kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa, Kata, Tarafa hadi Taifa; na

### 2.5 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango

**Mkakati Na. 1:** Kuimarisha uwezo kwa wataalam wa Serikali katika ngazi ya msingi (Ward Management Team) kwa kuwapa mafunzo, fedha, vitendea kazi na ofisi.

**Mkakati Na.2**: Kuimarisha uwezo kwa wataalam wa Serikali katika ngazi ya Halmashauri, Mikoa na Wizara ili kuwezesha utekelezaji wa mpango kwa ufanisi.

**Mkakati Na.3:** Kuongeza ushiriki wa Wananchi katika Shughuli za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira.

**Mkakati Na. 4:** Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA na na mifumo ya kisasa ya upashanaji wa habari

**Mkakati Na.5:** Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya mpango.

## 2.6 Shabaha za Mpango

Shabaha ya Mpango ni kuwa na:-

a) Wataalam wa ngazi za msingi (Tarafa 570, Kata 23,736,) waliojengewa uwezo kwa kuwapa vitendea kazi, vifaa, rasilimali fedha na mafunzo ifikapo Juni, 2024.
b) Kuimarisha ushiriki wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi katika Vijiji 12,318 na Mitaa 4263 ifikapo Juni 2024.
c) Kuongeza wigo wa mawasiliano kati ya Serikali na Wananchi kutoka asilimia 50 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 80 Juni 2024.

## 2.7 Viashiria vya Matokeo ya Mpango

### 2.7.1 Viashiria vya muda mfupi

(i) Ongezeko la Idadi ya Maafisa Tarafa waliojengewa uwezo katika utendaji kazi na utoaji huduma;
(ii) Ongezeka la Idadi ya Timu ya wataalam ngazi ya Kata waliojengewa uwezo katika utendaji kazi na utoaji wa huduma;

(iii) Ongezeka la Idadi ya miradi yenye tija na endelevu inayotokana na matakwa wananchi;

(iv) Ongezeko la Idadi ya wananchi wanaowasiliana na serikali kwa kutumia tovuti na mitandao ya kijamii;

(v) Ongezeko la wananchi wanaowasiliana na Serikali na Wananchi kutoka asilimia 50 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 80 Juni 2024

(vi) Vikao na Mikutano ya Vijiji na Mitaa kufanyika kila robo mwaka.

(vii) Kupungua kwa Idadi ya malalamiko na kero yanayopokelewa na kutatuliwa katika ngazi zote.

### 2.7.2 Viashiria vya Matokeo ya Muda Mrefu

a) Kuimarika kwa utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

b) Kuongezeka kwa moyo wa uzalendo wa kuipenda nchi kwa kufanya kazi kwa bidii na kujitolea.

## 2.8 Mbinu/Njia za Utekelezaji

(i) Kuimarisha Mifumo ya ushirikishwaji jamii ikiwemo Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ili kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi;

(ii) Kuimarisha utendaji kitimu (team work) ya watalaam ngazi ya Kata na kuwa na vikao vya tathmini kila wiki;

(iii) Kuwa na mfumo rahisi wa kielektroniki kwa kufuatilia ufanyikaji wa vikao ngazi ya kata;

(iv) Kuwa na mfumo wa kutoa mrejesho kuhusu utatuzi wa changamoto na kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

(v) Kuimarisha ufanyikaji wa vikao vya Kisheria katika ngazi ya Vijiji/Mtaa na Kata

(vi) Kuimarisha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA na upashanaji habari kwa njia za kisasa;

(vii) Kujaza nafasi za wataalam ngazi ya Tarafa na Kata (Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Mratibu wa Elimu Kata, Maafisa Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Waganga wakuu wa vituo vya afya;

(viii) Kutumia Taasisi zinazotoa mafunzo kwa viongozi na wataalamu katika ngazi ya msingi katika kutoa mafunzo ya kuboresha utendaji kazi vikiwepo Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru;

(ix) Kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Asasi za Kiraia katika huduma za jamii.

(x) Kutathmini utendaji kazi wa timu ya wataalam ngazi kata kupitia kadi alama (score card) na kutoa zawadi ya Kata.

# SURA YA TATU

# UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI

## 3.0 Utangulizi

Mpango umeandaliwa kwa ajili ya kuwezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo ngazi ya jamii na Taifa kwa kutumia rasilimali walizonazo katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kufuatilia shughuli/miradi ya maendeleo. Mpango unalenga kuchochea na kufanya mageuzi ya kifikra, mtazamo na kiutendaji kwa timu ya wataalam ngazi ya Kata ili kuboresha utendaji na utoaji wa huduma ngazi ya jamii katika sekta za elimu, afya, maji, nishati, mawasiliano, usafiri na usafirishaji, misitu na mazingira, ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii, uongozi na utawala bora. Aidha, maboresho yatawezesha kuwa na timu ya wataalamu wenye weledi, stadi, vifaa, vitendea kazi, rasilimali fedha na mifumo ya uratibu na ufuatiliaji na muda wa utekelezaji wake ni miaka mitatu (3) (mwaka 2022/2023 - 2025/2026).

Kama ilivyobainishwa mwanzo, uchambuzi wa hali halisi kupitia taarifa zilizopo OR TAMISEMI, Wizara za Kisekta na utafiti uliofanyika katika mikoa sita (6) ambayo ni Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha, Morogoro na Dar es Salaam umebainisha changamoto zifuatazo:-

a) Upungufu wa wataalam wakiwemo Watendaji wa Kata na Vijiji/Mtaa Maendeleo ya jamii katika ngazi ya msingi;
b) upungufu wa rasilimali fedha, vifaa na vitendea kazi kwa watendaji katika ngazi ya Mamlaka za serikali za Mitaa na ngazi ya msingi
c) Wataalam wa ngazi za msingi kutotumika vema katika ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi;

d) Uwezo mdogo wa wataalam wa ngazi za msingi kuwahudumia wananchi; na
e) Mawasiliano hafifu baina ya wananchi na serikali.

### 3.1 Utekelezaji wa Mpango

Maeneo ya utekelezaji wa Mpango yanajumuisha utatuzi wa changamoto zilizobainishwa katika utangulizi kama ifuatavyo:-

**(i) Kuwa na Rasilimali watu Inayotosheleza Kutekeleza** M**pango**

Mpango unakusudia kuziba mapengo ya watumishi ngazi ya msingi kwa kuajiri watumishi wapya na kufanya msawazo kwenye maeneo yenye ziada ya watumishi ukilinganisha na majukumu wanaotekeleza.

**(ii) Kuimarisha uwezo wa utendaji kazi wa wataalam ngazi ya msingi katika utoaji huduma**

Mpango katika eneo hili unalenga kujenga uwezo wa wataalam katika ngazi za Vijiji/Mitaa, Kata na Tarafa ili kuboresha utoaji wa huduma. Aidha, mpango utawezesha upatikanaji wa vifaa, vitendea kazi, vyombo vya usafiri,rasilimali fedha na mafunzo kwa wataalamu ngazi ya msingi.

Aidha, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na Chuo cha Utumishi wa Umma vitatumika kutoa stadi za uongozi, ushirikishaji jamii, wataalam na watendaji wa Serikali ili kuleta ufanisi katika majukumu yao pamoja na kuwapandikizia fikra za ujasiriamali na uzalendo.

**(iii) Kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi**

Ushirikishwaji jamii katika maamuzi, upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini katika masuala yanayohusu ustawi na maendeleo yao ni nyenzo muhimu ya kuwawezesha kuwa kitovu cha maendeleo yao. Vilevile, ushirikishwaji utawezesha kutambua wajibu wao na mchango wa Serikali katika maendeleo. Mpango shirikishi kwa Timu ya Wawezeshaji Ngazi ya Kata utaamsha ari ya jamii katika masuala ya uzalendo, moyo wa kujitolea, kufanya kazi kwa bidii, kuwajibika na kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi kuanzia ngazi ya jamii hadi Taifa.

**(iv) Kuimarisha Mawasiliano kati ya Wananchi na Serikali**

Mpango utahakikisha kuwa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi zinawafikia wananchi kila wakati kupitia vikao, mikutano na njia nyingine za mawasiliano kama mbao za matangazo, redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Pia, mifumo ya malalamiko na mrejesho wa kero za wananchi pamoja na ule wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango Shirikishi itahuishwa.

**(v) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA na mifumo ya kisasa ya upashanaji wa habari**

TEHAMA na Vyombo vya Habari ni nyenzo muhimu katika kuwawezesha wananchi kuwasiliana na Serikali na kupata mrejesho wa masuala mbalimbali yanayolenga kuchochea ustawi wao. Aidha, ili kuwezesha wananchi kuwa na mawasiliano yenye tija Serikali ina jukumu la kujenga uelewa wa wananchi kuhusu matumizi ya mifumo kama e-Mrejesho, iMIS, Helpdesks, Zungumza na Serikali (ZUSE), Tovuti za Wizara.

**(vi) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi na utoaji wa huduma katika ngazi ya msingi**

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utawezesha kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji pamoja na upatikanaji wa takwimu za awali ambazo zitasaidia kupata suluhu ya changamoto na maamuzi mbalimbali kuhusu mpango.

### 3.2 Matokeo ya Utekelezaji wa Mpango

Utekelezaji wa Mpango huu unatarajiwa kuleta matokeo yafuatayo:

I. Kuimarika kwa uwezo wa watendaji wa Serikali katika ngazi ya Msingi ya utoaji wa huduma bora kwa wananachi

II. Kuwepo kwa jamii yenye uwezo wa kutambua nafasi yake katika kutatua changamoto zinazoikabili kwa kutumia rasilimali zilizopo bila kuisubiri Serikali.

III. Kuongezeka kwa wananchi wenye uwezo wa kusimamia na kuelezea manufaa ya miradi ya maendeleo ngazi ya jamii na Kitaifa inayotekelezwa katika maeneo yao;

IV. Kuongezeka kwa wigo wa wananchi kuwasiliana na Serikali kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa na kukuza ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi na kijamii;

V. Kuongezeka kwa uwezo wa wataalam ngazi ya jamii wa kutumia TEHAMA kuibua na kutumia fursa zilizopo na kutatua changamoto za Kiuchumi, Kijamii, Kimazingira na Kiutamaduni;

VI. Kuimarika kwa uwezo wa viongozi wa Serikali za Mitaa na wananchi katika kuibua na kusimamia utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo;

Bangokitita la Mpango linapatikana kwenye **Kiambatisho Na. 1**

# SURA YA NNE

# GHARAMA ZA UTEKELEZAJI

## 4.0 Utangulizi

Gharama za Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo ngazi ya msingi, zimepangwa ili kubaini kiasi cha fedha kinachohitajika katika utekelezaji wa maeneo sita ya Mpango ambayo ni:-

i. Kuwa na rasilimali watu Inayotosheleza Kutekeleza Mpango;
ii. Kuimarisha uwezo wa utendaji kazi wa wataalam ngazi ya msingi katika utoaji huduma
iii. Kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi Kuimarisha Mawasiliano kati ya Wananchi na Serikali;
iv. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi na utoaji wahuduma katika ngazi ya msingi na
v. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA na mifumo ya kisasa ya upashanaji wa habari

## 4.1 Gharama za Utekelezaji wa Mpango

Jumla ya gharama za Mpango katika kipindi cha miaka mitatu inakadiriwa kuwa **Shilingi 184,620,350,000.00** kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni **Shilingi 88,590,540,000.00** na miradi ya maendeleo ni **Shilingi 96,029,810,000.00** kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4.** Utekelezaji wa Mpango utagharamiwa na Serikali na Wadau wa Maendeleo. Mpango kazi wa utekelezaji utaandaliwa katika kipindi cha mwanzoni mwa robo ya mwisho ya mwaka wa fedha husika. Aidha, bajeti itaandaliwa kwa kuzingatia rasilimali fedha zilizopatikana na kugawanywa kulingana na malengo mkakati na afua

zilizopangwa. Bangokitita la gharama za utekelezaji linapatikana kwenye **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4:** Gharama za Utekelezaji wa Mpango

| MATUMIZI | MWAKA | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/2023 | 2023/2024 | 2024/2025 | |
| Matumizi Mengineyo | 47,084,173,333.33 | 20,839,433,333.33 | 20,666,933,333.33 | **88,590,540,000.00** |
| Matumizi ya fedha za Maendeleo | 2,154,770,000.00 | 31,949,640,000.00 | 31,925,400,000.00 | **96,029,810,000.00** |
| **JUMLA KUU:** | **9,238,943,333.33** | **52,789,073,333.33** | **52,592,333,333.33** | **184,620,350,000.00** |

# SURA YA TANO

# MUUNDO WA KITAASISI NA URATIBU WA MPANGO

## 5.0 MUUNDO WA KAMATI

Muundo wa Kamati unajumuisha Ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri, Tarafa na Kata. Muundo huu umezitambua Kamati zitakazohusika ikiwemo Kamati ngazi ya Taifa zinazojumuisha Kamati ya Makatibu Wakuu na Kamati ya Wataalam; Kamati Ngazi ya Mkoa, Kamati Ngazi ya Halmashauri, Afisa Tarafa na Timu ya Wataalam ngazi ya Kata na Vijiji/Mtaa. Muundo wa kamati na majukumu yao ni kama yalivyoainishwa hapa chini:-

### 5.1 Kamati Makatibu Wakuu

Kamati hii itakuwa chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu – OR-TAMISEMI. Katibu Mkuu - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum atakuwa Katibu. Kamati Itajumuisha wajumbe wafuatao:- Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango; Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo; Katibu Mkuu Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Katibu Mkuu Mifugo na Uvuvi, Katibu Mkuu Wizara Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Katibu Mkuu Afya. Kamati hii itatoa Mwongozo na uratibu wa Kisera wa Mpango na itakutana mara mbili kwa mwaka.

Kamati itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kupokea na kupitia taarifa za utekelezaji wa Mpango kutoka kwenye Kamati ya Wataalam na kutoa mapendekezo kwa ajili ya maboresho;

(b) Kupitia na kupendekeza kuhusu mkakati wa mawasiliano katika ngazi ya msingi;

(c) Kuratibu upatikanaji wa rasilimali watu na fedha,vitendea kazi na vifaa kwa utekelezaji wa Mpango; na
(d) Kushauri Wizara za Kisekta kuhusu utekelezaji wa Mpango ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa wataalam wa sekta zao katika ngazi ya msingi.

### 5.2 Kamati ya Wataalam

Kamati hii itakuwa chini ya Uenyekiti wa Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa, OR-TAMISEMI na Katibu atakuwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Wajumbe watatakua ni Wakurugenzi watakaoteuliwa na katibu Mkuu katika Wizara zifuatazo: OR-TAMISEMI; Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum; Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Fedha na Mipango; Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Kilimo; Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Mifugo na Uvuvi; Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Afya. Kamati hii itakuwa pa ndiyo Sekretarieti ya Kamati ya Makatibu Wakuu na itakutana kila robo mwaka na kila inapohitajika.

Majukumu ya kamati yatakuwa yafuatayo:

(a) Kuandaa rasimu ya mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mpango;
(b) Kuratibu utekelezaji wa Mpango;
(c) Kutoa ushauri wa kiufundi kwa Kamati Tendaji;
(d) Kuwaendeleza na kuwapa mbinu za uhamasishaji na kusimamia maendeleo na mikakati mipya ya mawasiliano kwa wataalam katika ngazi ya Wilaya na Kata;
(e) Kuratibu uundwaji wa mfumo rahisi wa kieletroniki utakaohusiana na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango; na
(f) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Mpango kila robo mwaka.

### 5.3 Kamati ya Uratibu Ngazi ya Mkoa

Kamati ya Mkoa itaratibu afua zote za utekelezaji wa Mpango na itakuwa chini ya Uenyekiti wa Katibu Tawala wa Mkoa na Katibu Tawala Mipango na Uratibu atakuwa katibu. Wajumbe wa Kamati ya

Mkoa ni :- Katibu Tawala Msadizi Uchumi na Uzalishaji, Katibu Tawala Msaidizi wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Katibu Tawala Msaidizi Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Katibu Tawala Msaidizi Elimu, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, Mratibu wa O&OD iliyoboreshwa na Maendeleo ya Jamii. Kamati itakutana mara moja kila robo mwaka na kila inapohitajika.

Kamati itakutana mara moja kila robo mwaka na kila inapohitajika na itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha mipango na bajeti zote za Halmashauri zinajumuisha afua za Mpango**;**
(b) Kutoa msaada wa kiufundi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Mpango;
(c) Kuratibu utekelezaji wa Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ngazi ya Halmashauri; Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa mawasiliano;
(d) Kushirikisha wadau wa maendeleo ndani ya Mkoa kuhusu utekelezaji wa Mpango;
(e) Kuandaa taarifa za kila robo mwaka za Utekelezaji wa Mpango na kuwasilisha OR – TAMISEMI; na
(f) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango ngazi ya Wilaya.

### 5.4 Kamati ya Uratibu Ngazi ya Halmashauri

Katika ya ngazi ya Halmashauri Uenyekiti utakuwa chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri husika na Katibu atakuwa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. Wajumbe wa Kamati hii ni:- Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji, Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mkuu wa Idara ya Elimu ya Sekondari, Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi, Mkuu wa Idara ya Afya, Mkuu wa na Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini na Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. Kamati itakutana kila mwezi na wakati wowote itakapohitajika.

Kamati Ngazi ya Halmashauri itakuwa na Majukumu yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kuwa Bajeti inatengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango;
(b) Kujenga uwezo wa timu ya wawezeshaji ngazi ya kata katika kutekeleza Mpango;
(c) Kutekeleza Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo;
(d) Kutekeleza mkakati wa mawasiliano ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa timu ya wawezeshaji kuhusu matumizi ya TEHAMA na mifumo ya kisasa ya upashanaji wa habari;
(e) Kuratibu upatikanaji wa vitendea kazi na vifaa;
(f) Kutoa taarifa kwa wakati kuhusu utekelezaji wa Mpango kwenye Sekretarieti za Mikoa;
(g) Kuweka mazingira wezeshi ya wananchi kushiriki katika kujiletea maendeleo;
(h) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango katika Kata na Vijiji/Mtaa; na
(i) Kufanya masawazo wa rasilimaliwatu ndani ya Halmashauri ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Mpango

### 5.5 Ngazi ya Tarafa

Tarafa ni ngazi ya chini ya Wilaya na inaongozwa na Afisa Tarafa. Katika ngazi hii, haana watumishi zaidi ya Afisa Tarafa. Afisa Tarafa atakuwa ni kiungo kati ya Halmashauri na Kata katika utekelezaji wa Mpango na atashiriki vikao vya uratibu wa Mpango vya kila mwezi katika ngazi ya Halmashauri na kila baada ya wiki mbili katika ngazi ya Kata.

Afisa Tarafa atahusika:-

(a) Kufuatilia utekelezaji wa shughuli za mpango katika Kata zilizoko kwenye eneo lake
(b) Kusimamia utekelezaji wa mfumo fursa na vikwazo ulioboreshwa na kuhakikisha vikao vya timu ya Wataalamu ngazi ya Kata vinakaa
(c) Kuwa kiungo kati ya Halmashauri na Kata katika utekelezaji wa Mpango na atashiriki vikao vya uratibu wa Mpango vya kila robo mwaka katika ngazi ya Halmashauri na kila inapohitajika.

### 5.6 Timu ya Wataalam Ngazi ya Kata

Timu ya Wataalam itakuwa chini ya Uenyekiti wa Afisa Mtendaji wa Kata na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata atakuwa Katibu wa Kamati. Wajumbe wa Kamati watakuwa Kamati ya Wataalam wa Kata (Afisa Kilimo, Afisa Mifugo na Uvuvi, Mratibu Elimu Kata na Mganga Mkuu wa Kituo, Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa katika Kata husika na wataalamu wengine katika ngazi ya Kata). Kamati itakutana mara mbili kila mwezi kujadili mafanikio, changamoto na kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa Mpango.

Timu ya Wataalam ngazi ya Kata itafanya Majukumu yafutayo:-

(a) Kuamsha ari ya jamii kuhusu uzalendo, kufanya kazi bidii, kujitolea na kushiriki katika shughuli za maendeleo na miradi ili kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi;

(b) Kutekeleza Mfumo Ulioboreshwa wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo katika shughuli/miradi mbalimbali ya maendeleo ngazi ya jamii;

(c) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano ikiwa ni pamoja kutangaza mafanikio ya shughuli/miradi inayotekelezwa katika ngazi ya jamii;

(d) Kuibua fursa za kiuchumi katika ngazi ya msingi;

(e) Kuwezesha usimamizi wa pamoja katika kutekeleza shughuli na miradi ya maendeleo katika ngazi ya Vijiji/Mtaa;

(f) Kupokea na kubaini changamoto/kero mbalimbali kutoka kwenye Jamii na kuzitafutia ufumbuzi;

(g) Kuhimiza wajibu wa kila mwananchi kuchangia maendeleo ya nchi ikiwa ni pamoja na kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi;

(h) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango katika ngazi ya Kata na Vijiji/Mtaa; na

(i) Kutoa taarifa za utekelezaji kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kila robo mwaka.

# SURA YA SITA

# UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MPANGO

## 6.0 Utangulizi

Eneo la utekelezaji wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini litaimarisha mifumo iliyopo katika ngazi ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kupanga, kutekeleza na kutoa taarifa za utekelezaji wa Mpango. Ufuatiliaji na tathmini ya Mpango utaleta ufanisi kwenye utekelezaji wa afua katika ngazi zote. Ufuatiliaji huu utatoa taarifa na kushauri endapo kuna mahitaji ya kufanya marekebisho kwenye maeneo ya kimkakati na afua zake.

## 6.1 Malengo ya Ufuatialiji wa Mpango

Lengo kuu la ufuatiliaji ni kutoa nafasi ya majadiliano na maamuzi yanayohusu maboresho kulingana na takwimu zilizokusanywa wakati wa utekelezaji wa Mpango.

Malengo Mahsusi ya ufuatiliaji wa Mpango ni**:-**

i. Kuhakikisha malengo ya mpango yanafikiwa kama ilivyotarajiwa;

ii. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango ili kubaini maeneo yenye changamoto na kuboresha utekelezaji wake;

iii. Kuhakiksha Mpango unatekelezwa kulingana na rasilimali zilizotengwa; na

iv. Kuhamasisha utekelezaji wa Mpango na utoaji wa taarifa**.**

Ili kufanikisha malengo hayo, mifumo iliyopo ya ufuatiliaji inatakiwa kuimarishwa na kufungamanishwa na mipango mikakati ya ufutiliaji ya Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali, na kuonisha na mifumo ya ufuatiliaji ya kisekta na tathmini. Kwa kuwa Mpango huu

utahusishwa Wizara zaidi ya moja utaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu ambayo itahakikisha:

**i.** Kuna miongozo ya ufuatiliaji;

ii. Inawajengea watendaji na wataalamu uwezo wa utekelezaji wa mpango shirikishi wa Mawasiliano, ukusanyaji, uchakataji, uchambuzi wa takwimu na utoaji wa taarifa;

iii. Inawezesha tathmini ya pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango; na

iv. Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitakazowasilishwa na kujadiliwa kwenye mikutano ya mwaka katika ngazi ya taifa zimeunganishwa/zimeandaliwa.

Vilevile, kutakuwepo na ufuatiliaji katika kipindi cha nusu mwaka na mwaka kutathmini utendaji kazi na kutoa fursa ya kutafakari kuhusu mifano bora, changamoto na mafunzo yaliyopatikana. Tathmini ya jumla ya mpango itafanyika katika vipindi viwili kipindi cha kati cha utekelezaji wa Mpango na kipindi cha mwisho cha utekelezaji wa Mpango.

### 6.2 Viashiria na Shabaha

Ili kupima hatua za utekelezaji zilizofikiwa kwa kila shughuli iliyopangwa, viashiria vinavyozingatia ubora na idadi vimeandaliwa kwa kila eneo la utekelezaji. Utafiti wa awali utafanyika ili kubainisha takwimu zinazokosekana katika viashiria vinavyokuwa havina taarifa ya msingi.

### 6.3 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtiririko na Taarifa

Mtiririko wa takwimu na taarifa kutoka kwenye ngazi ya kijiji/Mtaa hadi ngazi ya Taifa kupitia OR TAMISEMI unauata mfumo ulioanishwa katika utaratibu wa kitaasisi. Mfumo wa mchanganuo wa matokeo ya mpango kazi umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3**

## *Kiambatisho Na.1*

**Jedwali Na.1: Mpango Kazi**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ***KIAMBATISHO NA. 1*** | | | | |
| **MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI 2022/23-2025/26** | | | | |
| **MKAKATI** | **SHABAHA** | **SHUGHULI** | **MUDA WA UTEKELEZAJI** | **WAHUSIKA** |
| ***LENGO NA 1*** | ***Kuimarisha uwezo wa wataalam wa Serikali kuanzia ngazi ya Mitaa/Vijiji, Kata, Tarafa, Halmashauri, Mkoa hadi Taifa katika kutoa huduma bora kwa wananchi*** | | | |
| **Mkakati Na. 1: Kuimarisha uwezo kwa wataalam wa Serikali katika ngazi ya msingi (Ward Management Team) kwa kuwapa mafunzo, fedha, vitendea kazi na ofisi.** | Wataalam wa ngazi za msingi (Tarafa 570, Kata 3,956* watalaam 6 = 23,736,) waliojengewa uwezo kwa kuwapa vitendea kazi, vifaa, rasilimali fedha na mafunzo ifikapo Juni, 2025 | **1.** Kuandaa Mpango wa mafunzo kwa wataalam katika ngazi ya msingi ifikapo Desemba, 2022. | Desemba,2022 | OR-TAMISEMI na WMJJWM |
| | | **2** Kutoa Mafunzo ya uimarishaji utendaji kazi na utoaji huduma ikiwemo matumizi ya mbinu shirikishi ya mfumo ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo na kuongeza uelewa wa Sera na Miongozo mbalimbali ifikapo Desemba, 2022. | Desemba, 2022 | OR-TAMISEMI WMJJWM, Wizara za Kisekta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **3.** Kuwezesha upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi kwa Watendaji na Wataalaam ngazi ya kata ikiwemo compyuta, printer, na vyombo vya usafiri (pikipiki) ifikapo Juni 2024. | 2022/23 – 2023/24 | OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,OR-MUUUB,WFM na Wizara za Kisekta |
| | | **4**. Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali watu katika ngazi ya Kata ifikapo Juni 2023 | 2022/23 – 2023/24 | OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,OR-MUUUB,WFM na Wizara za Kisekta |
| | | **3.** Kuwezesha Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kutoa stadi za Uongozi kwa viongozi na wataalam wa ngazi za msingi. | 2022/23 – 2024/25 | OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,OR-MUUUB,WFM |
| **Mkakati Na.2: Kuimarisha uwezo kwa wataalam wa Serikali katika ngazi ya Halmashauri, Mikoa na** | Kuongeza uwezo wa watalaam wa Halmashauri, Mikoa na Wizara kuratibu utekelezaji wa mpango ifikapo Juni,2024 | **1**.Kufanya vikao kazi vya kuongeza uelewa wa mpango | 2022/23 – 2023/24 | OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,OR-MUUUB,WFM |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Wizara ili kuwezesha utekelezaji wa mpango kwa ufanisi.** | | **2.** Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kama compyuta na usafiri kwa ajili ya shughuli za uratibu na ufuatiliaji | 2022/23 – 2024/25 | OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,OR-MUUUB,WFM |
| ***LENGO Na. 2:*** | ***Kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi*** | | | |
| **Mkakati Na. 3 Kuamsha Ari ya jamii kuhusu suala la Uzalendo, moyo wa kujitolea na kufanya kazi kwa bidii na kushiriki katika shughuli za Kijamii na Kiuchumi** | Ushiriki wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi kuongeza kufikia Juni,2022 | 1.Kuwezesha Wananchi katika kuibua, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi. | 2022/23 -i 2025/26 | Timu ya Wawezeshaji ngazi ya Kata |
| | | **2.** Kuamsha ari ya jamii kuhusu suala la uzalendo, moyo wa kujitolea na kufanya kazi kwa bidii katika shughuli za kijamii na kiuchumi. | 2022/23 - 2025/26 | Timu ya Wawezeshaji ngazi ya Kata |
| ***LENGO Na. 3:*** | ***Kuongeza wigo wa wananchi kuwasiliana na Serikali kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa, Kata, Tarafa hadi Taifa*** | | | |
| **Mkakati Na. 4: Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA na mifumo ya kisasa ya** | Wigo wa wananchi kuwasiliana na Serikali kuongezeka Kufikia Juni, 2024 | **1.**Kuhuisha mifumo ya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa wananchi | Juni, 2023 | OR – TAMISEMI |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **upashanaji habari.** | | **2**. Kuhuisha Mfumo wa utatuzi wa -malalamiko/kero kwa wananchi | Juni, 2023 | OR- MUUUB |
| | | **3.** Kujenga uwezo wa timu ya wataalam ngazi ya kata juu ya mifumo ya usimamizi na utoaji taarifa | Juni 2023 | WHMTH, WMJJW, |
| | | **4**. Kutoa Elimu kwa Wananchi kuhusu matumizi ya Mifumo ya Mawasiliano kati ya Wananchi na Serikali (mfano: e-Mrejesho, iMIS, Helpdesks, Zungumza na Serikali (ZUSE), Tovuti na mitandao ya kijamii | Juni,2023 | OR- TAMISEMI, WHMTH, OR-MUUUB |
| **Mkakati: 5 Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya mpango** | Kuimarika kwa ufuatiliaji na tathimini kufikia Juni,2024 | **1**. Kuunda Mfumo wa Kieletroniki wa ufuatiliaji na tathimini wa utendaji kazi na utoaji wa huduma ngazi ya msingi | Juni, 2023 | OR – TAMISEMI, WMJJW, |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **2.** Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango Shirikishi wa Kuimarisha Utendaji Kazi na utoaji wa huduma ngazi ya Kata | 2022/23 – 2024/25 | OWM–Sera, Uratibu na Bunge, OR – TAMISEMI WMJJW WHMTH |
| | | **3**. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mpango | 2022/23 – 2024/25 | Timu ya Waweshaji Ngazi ya Kata |
| | | **4.** Kuratibu vikao vya tathimini ngazi ya Taifa kuhusu mpango wa utendaji kazi na utoaji wa huduma ngazi ya kata kwa jamii | 2022/23 – 2025/26 | OR – TAMISEMI WMJJW, |

## Kiambatisho Na.2

### Jedwali Na.2: Bajeti ya Mpango

| BAJETI YA MPANGO WA TAIFA WA KUHAMASISHA NA KUSIMAMIA MAENDELEO NGAZI YA MSINGI | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **LENGO/ MKAKATI/ SHABAHA** | **SHUGHULI** | **MAELEZO** | **KIPIMO** | **IDADI YA WATU/ VITU** | **BEI** | **SIKU/ LITA** | **JUMLA** | **MUDA WA UTEKELE ZAJI** | **WAHUSIKA** |
| ***LENGO NA 1 Kuimarisha uwezo wa wataalam wa Serikali kuanzia ngazi ya Mitaa/Vijiji, Kata, Tarafa, Halmashauri, Mkoa hadi Taifa katika kutoa huduma bora kwa wananchi*** | | | | | | | | | |
| ***Mkakati Na. 1: Kuimarisha uwezo kwa wataalam wa Serikali katika ngazi ya msingi (Ward Management Team) kwa kuwapa mafunzo, fedha, vitendea kazi na ofisi.*** | | | | | | | | | |
| **Wataalam wa ngazi za msingi (Tarafa 570, Kata 3,956 x 23,736,) waliojengewa uwezo kwa kuwapa vitendea kazi, vifaa, rasilimali fedha na** | **1.** Kuandaa Mpango wa mafunzo kwa wataalam katika ngazi ya msingi ifikapo Desemba, 2022. | Shajala | Seti | 4 | 100,000 | 1 | 400,000.0 | Disemba ,2022 | **OR-TAMISEMI WMJJWMI** |
| | | Posho kwa wataalam | Mtu | 8 | 170,000 | 1 | 1,360,000.0 | | |
| | | Ukumbi | Siku | 5 | 250,000 | 1 | 1,250,000.0 | | |
| | | Viburudisho | mtu | 8 | 20,000 | 1 | 160,000.0 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **mafunzo ifikapo Juni, 2025** | | Kuzalisha vitabu vya kujifunzia | mtu | 24,306 | 10,000 | 1 | 243,060,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **246,230,000.0** | | |
| | **2** Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa Mafunzo ya uimarishaji utendaji kazi na utoaji huduma ikiwemo matumizi ya mbinu shirikishi ya mfumo ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo na kuongeza uelewa wa Sera na Miongozo mbalimbali ifikapo Desemba, 2022. | Shajala kwa washiriki ( washiriki 2@LGAS na washiriki 2@RS) | Mtu | 420 | 150,000 | 3 | 189,000,000.0 | Disemba , 2022 | **OR-TAMISEMI WMJJWM, Wizara za Kisekta** |
| | | Posho ya wawezeshaji | Mtu | 21 | 220,000 | 3 | 13,860,000.0 | | |
| | | Posho kwa Madereva wa Viongozi | Mtu | 5 | 150,000 | 3 | 2,250,000.0 | | |
| | | Viburudisho | Siku | 446 | 20,000 | 3 | 26,760,000.0 | | |
| | | Ukumbi | mtu | 3 | 400,000 | 3 | 3,600,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **235,470,000.0** | | |
| | **3** Kutoa Mafunzo ya uimarishaji | Shajala kwa washiriki | Seti | 23,736 | 5,000 | 1 | 118,680,000.0 | Disemba , 2022 | **OR-TAMISEMI WMJJWM,** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | utendaji kazi na utoaji huduma ikiwemo matumizi ya mbinu shirikishi ya mfumo ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo na kuongeza uelewa wa Sera na Miongozo mbalimbali ifikapo Desemba, 2022. | Posho kwa wawezeshaji wa Mkoa | Mtu | 420 | 70,000 | 8 | 235,200,000.0 | | **Wizara za Kisekta** |
| | | Posho kwa wataalam(kata 3,956 X Wataalam ngazi ya kata 6 X SIKU 6) | Mtu | 23,736 | 50,000 | 8 | 9,494,400,000.0 | | |
| | | Ukumbi | siku | 184 | 150,000 | 8 | 220,800,000.0 | | |
| | | Viburudisho | mtu | 47,892 | 20,000 | 8 | 7,662,720,000.0 | | |
| | | **Jum la Ndogo** | | | | | **17,731,800,000.0** | | |
| | **4.** Kuwezesha upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi kwa Watendaji na Wataalaam ngazi ya kata ikiwemo compture, | Pikipiki | Kila moja | 1,134 | 7,000,000 | 1 | 7,938,000,000.0 | 2022/23 – 2023/24 | **OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,OR-MUUUBWFM na Wizara za Kisekta** |
| | | Compture | Kila moja | 3,956 | 1,000,000 | 1 | 3,956,000,000.0 | | |
| | | Printa | Kila moja | 3,956 | 700,000 | 1 | 2,769,200,000.0 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | printer, na vyombo vya usafiri pikpiki | shajala | Kila moja | 3,956 | 50,000 | 4 | 791,200,000.0 | | |
| | | wino | Kila moja | 3,956 | 150,000 | 2 | 1,186,800,000.0 | | |
| | | **Jum la Ndogo** | | | | | **16,641,200,000.0** | | |
| | **5.** Kuwezesha upatikanaji wa ofisi | Ofisi za Tarafa | Kila moja | 337 | 30,000,000 | 1 | 10,110,000,000.0 | 2022/23 – 2023/24 | **OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,** |
| | | Ofisi za kata | Kila moja | 1,965 | 25,000,000 | 1 | 49,125,000,000.0 | | |
| | | **Jum la Ndogo** | | | | | **59,235,000,000.0** | | |
| | 6. Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali watu katika ngazi ya kata | Upungufu wa wataalamu ngazi ya Kata | | | | | | 2022/23 – 2023/24 | **OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH, OR MUUUB WFM na Wizara za Kisekta** |
| | **7.** Kuwezesha | Shajala | Seti | | | 1 | | 2022/23 | **WMJJW,** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kutoa stadi za Uongozi kwa viongozi na wataalam wa ngazi za msingi. | | | 15 | 10,000 | | 150,000.0 | – 2024/25 | **OR – TAMISEMI, OR-Utumishi wa Umma na Utawala Bora.** |
| | | Posho kwa waalikwa-katika vyuo | Mtu | 11 | 170,000 | 2 | 3,740,000.0 | | |
| | | Posho kwa wawezeshaji | Mtu | 8 | 170,000 | 2 | 2,720,000.0 | | |
| | | Posho kwa viongozi | Mtu | 5 | 220,000 | 2 | 2,200,000.0 | | |
| | | Posho kwa madereva | Mtu | 14 | 150,000 | 2 | 4,200,000.0 | | |
| | | Ukumbi | Siku | 1 | 400,000 | 2 | 800,000.0 | | |
| | | Viburudisho | mtu | 38 | 20,000 | 1 | 760,000.0 | | |
| | | Kuzalisha vitabu vya kujifunzia | mtu | 11 | 10,000 | 1 | 110,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **14,680,000.0** | | |
| **Mkakati Na.2:Kuimarisha uwezo kwa wataalam wa Serikali katika ngazi ya Halmashauri, Mikoa na Wizara ili kuwezesha utekelezaji wa mpango kwa ufanisi.** | | | | | | | | | |
| **Kuongeza uwezo wa** | **1**.Kufanya vikao kazi vya | Shajala | Seti | 400 | 10,000 | 1 | 4,000,000.0 | 2022/23 – | **OR-TAMISEMI** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **watalaam wa Halmashauri, Mikoa na Wizara kuratibu utekelezaji wa mpango ifikapo Juni,2024** | kuongeza uelewa wa mpango | Posho kwa wataalam | Mtu | 400 | 70,000 | 2 | 56,000,000.0 | 2023/24 | **WMJJWM, WHMTH, OR-MUUUB WFM** |
| | | Viburudisho | mtu | 400 | 20,000 | 1 | 8,000,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **68,000,000.0** | | |
| | 2.Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kama compyuta na usafiri kwa ajili ya shughuli za uratibu na ufuatiliaji | Mikoa | Kila moja | 26 | 50,000, 000 | 1 | 1,300,000,000.0 | 2022/23 – 2023/24 | **OR-TAMISEMI WMJJWM, WHMTH,** |
| | | Halmashauri | Kila moja | 184 | 50,000, 000 | 2 | 18,400,000,000.0 | | |
| | | Wizara | Kila moja | 4 | 50,000, 000 | 1 | 200,000,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **19,900,000,000.00** | | |
| ***LENGO Na. 2:*** | ***Kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kijamii na kiuchumi*** | | | | | | | | |
| ***Mkakati Na. 3 Kuamsha Ari ya jamii kuhusu suala la Uzalendo, moyo wa kujitolea na kufanya kazi kwa bidii na kushiriki katika shughuli za Kijamii na Kiuchumi*** | | | | | | | | | |
| | 1.Kuwezesha Wananchi katika kuibua, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na | Mafuta | Lita | 3,596 | 3,500 | 400 | 5,034,400,000.0 | | **Timu ya Uwezeshaji ya Kata** |
| | | Posho ya kujikimu kwa | Mtu | 23,736 | 50,000 | 48 | 56,966,400,000.0 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi. | wataalam | | | | | | | |
| | | **Jumla** | | | | | **62,000,800,000.0** | | |
| | 2. Kuamsha ari ya jamii kuhusu suala la uzalendo, moyo wa kujitolea na kufanya kazi kwa bidii katika shughuli za kijamii na kiuchumi. | Shajala | Seti | 3,596 | 50,000 | 4 | 719,200,000.0 | Disemba ,2022 | **Timu ya Uwezeshaji ya Kata** |
| | | Mafuta | Lita | 3,596 | 3,500 | 400 | 5,034,400,000.0 | | |
| | | wino | seti | 3,596 | 150,000 | 4 | 2,157,600,000.0 | | |
| | | Posho ya masaa ya ziada | mtu | 3,596 | 50,000 | 16 | 118,680,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **8,029,880,000.0** | | |
| ***Kuongeza wigo wa wananchi kuwasiliana na Serikali kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa, Kata, Tarafa hadi Taifa*** | | | | | | | | | |
| ***Mkakati Na. 4:Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA na Vyombo vya Habari kufikisha taarifa kwa umma na kuwezesha wananchi kuwasiliana na Serikali.*** | | | | | | | | | |
| **Wigo wa wananchi kuwasiliana na Serikali kuongezeka Kufikia Juni, 2024** | 1.Kuhuisha mifumo ya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa | Shajala | Seti | 1 | 50,000 | 4 | 200,000.0 | Januari,2 022 | **WMJJW, OR – TAMISEMI,** |
| | | Ukumbi | Siku | 1 | 400,000 | 7 | 2,800,000.0 | | |
| | | Posho kwa Wataalam | Mtu | 15 | 170,000 | 7 | 17,850,000.0 | | |
| | | Viburudisho | mtu | 15 | 20,000 | 7 | 2,100,000.0 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | wananchi | Kuzalisha vitabu vya Viongozi vya maboresho ya mafumo | mtu | 1 | 10,000 | 20 | 200,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **23,150,000.0** | | |
| | 2. Kuhuisha Mfumo wa utatuzi wa - malalamiko/kero kwa wananchi | Shajala | Seti | 1 | 50,000 | 4 | 200,000.0 | Januari,2 022 | **OR-TAMISEMI WMJJWM na Wizara za Kisekta OR-MUUUB WFM** |
| | | Ukumbi | Siku | 1 | 400,000 | 7 | 2,800,000.0 | | |
| | | Posho kwa Wataalam | Mtu | 15 | 170,000 | 7 | 17,850,000.0 | | |
| | | Viburudisho | mtu | 15 | 20,000 | 7 | 2,100,000.0 | | |
| | | Kuzalisha vitabu vya Viongozi vya maboresho ya mafumo | mtu | 1 | 10,000 | 20 | 200,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **23,150,000.0** | | |
| | 3. Kujenga uwezo wa timu ya wataalam ngazi ya kata | Shajala | Seti | 1 | 50,000 | 10 | 500,000.0 | Machi,20 22 | **OR-TAMISEMI WMJJWM na Wizara** |
| | | Wino | Seti | 1 | 120,000 | 4 | 480,000.0 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | juu ya mifumo ya usimamizi na utoaji taarifa | Posho masaa ya ziada ya kuandaa miongozo ya maboresho | mtu | 6 | 70,000 | 15 | 6,300,000.0 | | **za Kisekta OR-MUUUB WFM** |
| | | Kuzalisha vitabu vya Viongozi vya maboresho ya mafumo | mtu | 1 | 10,000 | 3,956 | 39,560,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **46,840,000.0** | | |
| | **4**. Kutoa Elimu kwa Wananchi kuhusu matumizi ya Mifumo ya Mawasiliano kati ya Wananchi na Serikali (mfano: e-Mrejesho, iMIS, Helpdesks, Zungumza na Serikali (ZUSE), Tovuti na mitandao ya kijamii | Gharama ya matangazo | Kila moja | 184 | 200,000 | 4 | 147,200,000.0 | Disemba ,2022 hadi Juni,2023 | **OR-TAMISEMI WMJJWM na Wizara za Kisekta OR-MUUUB WFM** |
| | | gharama ya vipeperushi | Kila moja | 3,956 | 500 | 100 | 197,800,000.0 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Jumla ngogo** | | | | | **345,000,000.0** | | |
| **Mkakati: 5 Kuimarisha ufuatiliaji na tahimini ya mpango** | | | | | | | | | |
| **Kuimarika kwa ufuatiliaji na tathimini kufikia Juni,2024** | **1**. Kuunda Mfumo wa Kieletroniki wa ufuatiliaji na tathimini wa ya utendaji kazi na utoaji wa huduma ngazi ya msingi | Shajala | Seti | 1 | 50,000 | 4 | 200,000.0 | Januari,2 022 | **WMJJW, OR – TAMISEMI,** |
| | | Ukumbi | Siku | 1 | 400,000 | 7 | 2,800,000.0 | | |
| | | Posho kwa Wataalam | Mtu | 15 | 170,000 | 7 | 17,850,000.0 | | |
| | | Viburudisho | mtu | 15 | 20,000 | 7 | 2,100,000.0 | | |
| | | Kuzalisha vitabu vya Viongozi vya maboresho ya mafumo | mtu | 1 | 10,000 | 20 | 200,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **23,150,000.0** | | |
| | **2.** Kuwezesha Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango Shirikishi uimarishaji utendaji kazi na utoaji wa | Shajala | Seti | 20 | 50,000 | 4 | 4,000,000.0 | 2022/23 – 2024s/25 | **WMJJW, OR – TAMISEMI, WHMTH, OWM – Sera, Uratibu na Bunge.** |
| | | Mafuta | Lita | 8 | 3,500 | 400 | 11,200,000.0 | | |
| | | Posho ya kujikimu kwa wataalam | Mtu | 13 | 170,000 | 8 | 17,680,000.0 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | huduma ngazi ya kata | Posho kwa Viongozi | Mtu | 5 | 150,000 | 8 | 6,000,000.0 | | |
| | | Posho kwa Madereva | Mtu | 8 | 150,000 | 8 | 9,600,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **48,480,000.0** | | |
| | **3**. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mpango | Shajala | Seti | 2 | 50,000 | 4 | 400,000.0 | 2022/23 – 2024/25 | **Maafisa Tarafa, Maafisa Watendaji kata, Kijiji/Mtaa** |
| | | wino | Mtu | 2 | 120,000 | 4 | 960,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **1,360,000.0** | **-** | **-** |
| | **4.** Kuratibu vikao vya tathimini ngazi ya Taifa kuhusu mpango wa utendaji kazi na utoaji wa huduma ngazi ya kata kwa jamii | Shajala | Seti | 2 | 50,000 | 4 | 400,000.0 | 2022/23 – 2025/2026 | **WMJJW, OR – TAMISEMI,** |
| | | wino | Mtu | 2 | 120,000 | 4 | 960,000.0 | | |
| | | Viburudisho | mtu | 40 | 20,000 | 6 | 4,800,000.0 | | |
| | | **Jumla** | | | | | **6,160,000.0** | | |
| | | **Jumla Kuu** | | | | | **184,620,350,000.0** | **-** | **-** |

## *Kiambatatisho Na 3*

### Jedwali Na. 1: Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini

| **Na** | **Kiashiria** | **Maelezo ya kiashiria** | **Takwimu msingi** | | **Thamani ya kiashiria cha shabaha kwa mwaka** | | | | | **Njia za Ukusanyaji na uchambuzi wa Taarifa** | | | **Njia ya uthibiti shaji** | **Utoaji wa taarifa ni kwa muda gani** | **Mhusi ka** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Tare he | Tham ani | 1 | 2 | 3 | | | Chanzo cha taarifa | Nyenzo na njia za Kukusan ya taarifa | Muda wa Ukusan yaji wa taarifa | | | |
| | Asilimia ya Watendaji kata waliojenge wa uwezo katika nyanja mbalimbali zinazoleng a kuboresha Mawasilia no kati | Kiashiria hiki kina lengo la kupima asilimia ya Watendaji wa kata waliopata mafunzo.<br>Kiashiria hiki kitapimwa | 202 3 | 0% | 100 % | na | na | | | OR - TAMIS EMI | Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | Uwepo wa Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | OR - TAMIS EMI |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | yao na wananchi | kwa (x/y)*100 ambapo ‘x’ ni Watendaji wa kata waliopata mafunzo na ‘y’ ni Jumla ya Watendaji kata nchini. | | | | | | | | | | | | | |
| 2. | Asilimia ya Watendaji wa vijiji waliojenge wa uwezo katika nyanja mbalimbali zinazoleng a kuboresha Mawasilia no kati yao na wananchi | Kiashiria hiki kina lengo la kupima asilimia ya Watendaji wa kijiji waliopata mafunzo.<br>Kiashiria hiki kitapimwa kwa (x/y)*100 ambapo ‘x’ ni | 2023 | 0% | 100% | na | | | | OR - TAMIS EMI | Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | Uwepo wa Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | OR - TAMIS EMI |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watendaji wa kijiji waliopata mafunzo na ‘y’ ni Jumla ya Watendaji wa vijiji nchini. | | | | | | | | | | | | |
| | Asilimia ya Watendaji wa Mitaa waliojengewa uwezo katika nyanja mbalimbali zinazolenga kuboresha Mawasilia no kati yao na wananchi | Kiashiria hiki kina lengo la kupima asilimia ya Watendaji wa Mitaa waliopata mafunzo.<br>Kiashiria hiki kitapimwa kwa (x/y)*100 ambapo ‘x’ ni Watendaji wa mitaa | 2023 | 0% | 100% | na | | | | OR - TAMISEMI | Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | Uwepo wa Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | OR - TAMISEMI |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | waliopata mafunzo na ‘y’ ni Jumla ya Watendaji wa Mitaa nchini. | | | | | | | | | | | | | |
| **4.** | Asilimia ya Wataalam wa ngazi za msingi waliojengewa uwezo katika nyanja mbalimbali zinazolenga kuboresha Mawasilia no kati yao na wananchi | Kiashiria hiki kina lengo la kupima asilimia ya Wataalam wa ngazi za msingi waliojengewa uwezo.<br>Kiashiria hiki kitapimwa kwa (x/y)*100 ambapo ‘x’ ni Wataalam wa ngazi za msingi | 2023 | 100% | na | na | | | | OR - TAMISEMI | Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | Uwepo wa Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | DLG |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | waliojengewa uwezo ‘y’ ni Jumla ya Wataalam wa ngazi za msingi nchini | | | | | | | | | | | | | |
| **5.** | Idadi ya wananchi wanaotembelea tovuti, mitandao ya kijamii na blogu za taasisi za serikali | Kiashiria hiki kina lengo la kupima asilimia ya wananchi wanaotembelea tovuti, mitandao ya kijamii na blogu za taasisi za serikali<br><br>Kiashiria hiki kitapimwa kwa (x/y)*100 ambapo ‘x’ ni idadi ya | 2023 | 100% | na | na | | | | WHMTH | Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | Uwepo wa Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | HGCU |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | wananchi wanaotembalea tovuti, Mitandao ya kijamii na blogu za taasisi za serikali na 'y' ni jumla ya wanachi nchini | | | | | | | | | | | | |
| **6.** | Mfumo wa uratibu wa shughuli za kijamii, kiuchumi kwa ngazi ya msingi ulioandaliwa | | 2023 | 0% | 50% | 50% | | | | OR – TAMISEMI/MAENDELEO YA JAMII | Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | Uwepo wa Taarifa za Mafunzo | Nusu Mwaka | DLG/DCD |
| **7.** | Uelewa wa wananchi kuhusu utekelezaji wa shughuli za | Kiashiria hiki kina lengo la kupima uelewa wa wananchi kuhusu utekelezaji wa | | | | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali. | shughuli/miradi ya serikali<br><br>Kiashiria hiki kitapimwa kwa kufanya u***tafiti ambapo tutapata wenye uelewa wa juu, kati na chini*** | | | | | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **8.** | Ubora wa huduma zinazotolewa na Serikali (Mtazamo wa wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na serikali) | Kiashiria hiki kinalenga kupima huduma zinazotolewa na Serikali kwa wananchi<br>Kiashiria hiki kitapimwa kwa kutumia (secondary data) | | | | | | | | | | | | | | |

Imeandaliwa Na:

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Rais TAMISEMI